Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2026

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE TAREHE 21-31 OKTOBA, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhohofika. Hali hii ilisababisha sehemu ya ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kubaki kusini na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) lilikuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonesia). Hali hii iliimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale ya nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 OKTOBA, 2026

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na Magharibi mwa nchi; na vipindi mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2026

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika, wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha sehemu ya ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kubaki kusini, na kuwepo katika maeneo ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na maeneo machache ya kati na nyanda za juu kusini magharibi. Vilevile, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Africa

Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani kuliko lile la eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi (pwani ya Indonecia). Hali hii inatarajiwa kuimarisha kuvuma kwa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu na yale yaliyoko nyanda za juu kaskazini mashariki na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 NOVEMBA, 2026

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Vipindi vya Mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngururumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA